Makala

بسم الله الرحمن الرحيم

## Umuhimu wa Kimkakati wa Siasa za Kijiografia za Sudan

**(Imetafsiriwa)**

Sudan ni nchi yenye umuhimu mkubwa wa kisiasa za kijiografia, unaotokana na ardhi yake kubwa, maliasili nyingi, na eneo ambalo linaiweka kitovu cha baadhi ya njia muhimu zaidi za kibiashara na kisiasa duniani. Licha ya kukabiliwa na miongo kadhaa ya ukosefu wa utulivu wa kisiasa, Sudan inasalia kuwa kitovu cha maslahi kwa dola zenye nguvu za kieneo na kimataifa kutokana na nafasi yake ya kimkakati na uwezo wake ambao haujatumiwa. Umuhimu wake sio wa kisasa tu bali pia wa kihistoria, haswa katika zama ambazo ilikuwa sehemu ya Khilafah kubwa zaidi ya Kiislamu, ambapo ilichukua nafasi muhimu katika kuunganisha na kuimarisha ulimwengu mpana wa Kiislamu. Na umuhimu wake utabaki mbeleni, Khilafah itakaporegea.

Nafasi ya kijiografia ya Sudan ni moja ya rasilimali zake kuu za kimkakati. Ikiwa kaskazini-mashariki mwa Afrika, Sudan inapakana na nchi saba; Misri, Libya, Chad, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Sudan Kusini, Ethiopia, na Eritrea. Hii inafanya kuwa kiungo cha kati kati ya Afrika Kaskazini, eneo la Sahel, na Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Pia inajivunia ukanda wa pwani muhimu kando ya Bahari Nyekundu, moja kwa moja kutoka Rasi ya Arabia na karibu na Mlango-Bahari wa Bab al-Mandeb, mojawapo ya vituo muhimu zaidi vya kukokota baharini duniani.

Mlango Bahari wa Bab al-Mandeb unaunganisha Bahari Nyekundu na Ghuba ya Aden na Bahari ya Arabia, na kuifanya kuwa ukanda muhimu wa biashara ya kimataifa na usafirishaji wa mafuta. Takriban 10% ya mafuta ya baharini duniani hupitia njia hii nyembamba. Ukaribu wa Sudan kwenye njia hii ya maji unaifanya kuwa eneo linalohitajika kimkakati kwa dola zenye nguvu duniani zinazotafuta ushawishi juu ya njia za baharini na vifaa vya majini. Udhibiti au muungano na Sudan unaweza kutoa manufaa makubwa katika kudhibiti usalama wa Bahari Nyekundu na mtiririko wa biashara kati ya Asia, Ulaya na Afrika.

Zaidi ya hayo, Sudan ina utajiri mkubwa wa maliasili ambayo kwa kiasi kikubwa inainua thamani yake ya kijiografia na kisiasa. Ni mojawapo ya wazalishaji wakubwa wa dhahabu barani Afrika, na utajiri wake wa madini ni pamoja na chromium, manganese, zinc, mgodi wa chuma, na urani. Licha ya kujitenga kwa Sudan Kusini mwaka 2011, ambayo ilichukua sehemu kubwa ya maeneo ya mafuta, Sudan ingali na akiba kubwa ya mafuta na gesi, haswa mashariki na maeneo ya mipakani.

Zaidi ya hayo, Sudan ina maeneo makubwa ya ardhi ya kilimo na ni nyumbani kwa Nile ya Bluu na Nyeupe, na kuipa uwezo mkubwa wa kilimo na uzalishaji wa chakula. Imeonekana kwa muda mrefu kama “kapu la chakula” linalowezekana kwa Afrika na ulimwengu wa Kiarabu. Kwa miundombinu na utawala bora, Sudan inaweza kucheza dori muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula katika kanda.

Mbali na jiografia na rasilimali zake, thamani kubwaya kimkakati ya Sudan iko katika ushawishi wake ndani ya nyanja za kisiasa za Kiafrika na Kiarabu. Inatumika kama daraja la kitamaduni na kiuchumi kati ya Waarabu Kaskazini mwa Afrika na maeneo yenye Waislamu wengi katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Nafasi hii inaifanya kuwa mhusika muhimu katika diplomasia ya kikanda na katika miradi mipana inayolenga ushirikiano wa kiuchumi au umoja wa kisiasa.

Dola zenye nguvu duniani kama vile Marekani, China, Urusi, na wachezaji wa kikanda kama vile Dola za Ghuba na Uturuki zote zimeonyesha nia ya Sudan, iwe kupitia ushirikiano wa kijeshi, uwekezaji wa kiuchumi, au ushirikiano wa kisiasa. Ukanda wa Bahari Nyekundu unazidi kuwa wa kijeshi, na eneo la Sudan mara nyingi liko katikati ya mashindano haya. Bandari za nchi, anga, na wilaya hutoa fursa za kimkakati za ushawishi, haswa kwa kuzingatia mabadiliko ya miungano ya kimataifa na kupungua kwa udhibiti wa Magharibi katika maeneo fulani.

Umuhimu wa kimkakati na wa kirasilimali wa Sudan ulidhihirika hata ilipokuwa sehemu ya Khilafah kubwa ya Kiislamu. Chini ya Khilafah ya Uthmani, Sudan ilitumika kama mpaka muhimu wa ulimwengu wa Kiislamu. Bandari zake za Bahari Nyekundu zilikuwa muhimu kwa safari za kibiashara na kidini kati ya Afrika na Rasi ya Arabia, kuwezesha njia za mahujaji na ubadilishanaji wa kiuchumi katika Ummah.

Ardhi yenye rutuba na utajiri wa madini ya Sudan ilisaidia maendeleo ya ndani pamoja na biashara ya kikanda, na kuunganishwa kwake katika Khilafah kuliiruhusu kufaidika na kuchangia katika mfumo mpana wa uchumi na sheria ya Kiislamu. Katika kipindi hiki, utawala wa Kiislamu uliunganisha jamii na makabila mbalimbali chini ya bendera ya Uislamu, kutekeleza Sharia na kukuza haki na utulivu. Nafasi ya Sudan kama kituo cha kusini mwa Khilafah iliiwezesha kutumika kama kituo cha uzinduzi wa mawasiliano ya Kiislamu katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, na kuimarisha umoja wa kifikra na kiroho wa ulimwengu wa Kiislamu.

Uwezo wote mkubwa wa kimkakati na wa kirasilimali wa Sudan unaweza tu kutumiwa kwa njia ipasavyo na kwa haki chini ya Dola ya Kiislamu-Khilafah. Ni kupitia tu utabikishaji wa mfumo wa Kiislamu, unaoegemezwa juu ya Qur'an na Sunnah, ndipo utajiri, jiografia na ushawishi wa Sudan unaweza kusimamiwa kwa njia ambayo inahudumia maslahi ya watu wake na Ummah mpana zaidi. Kukosekana kwa utulivu wa kisiasa mara kwa mara, kuporomoka kwa uchumi, kuingiliwa na nchi za kigeni, na mgawanyiko wa ndani ambao Sudan imekumbwa na matokeo ya moja kwa moja ya kutokuwepo Khilafah. Bila ya uongozi mmoja wa Kiislamu unaotawala kwa sheria ya Mwenyezi Mungu, nchi hii inasalia katika hatari ya kunyonywa na dola za kigeni na kudanganywa na makundi ya kisekula, kikabila au kimfumo. Khilafah ingehakikisha ulinzi wa ubwana wa Sudan, kuwaunganisha watu wake chini ya itikadi moja, na kuelekeza nafasi yake ya kimkakati na utajiri wa kimaumbile kwenye kuinua ulimwengu mzima wa Kiislamu, huru kutokana na ushawishi wa kikoloni na ghasia za ndani.

**#SudanCrisis** **#أزمة_السودان**

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**
**Sumaya Bint Khayyat**